

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 55 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** SEPTEMBER 2025

NAIBU KATIBU WAKUU OR- TAMISEMI WATEMBELEA BANDA LA TSC SIKU YA KILELE CHA NANENANE



Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI anayeshughulikia Serikali za Mitaa, Bw. Sospeter Mtswale, akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la TSC katika maonesho ya Nanenane kitaifa jijini Dodoma.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

UMUHIMU WA WALIMU KUSHIRIKI KWENYE UCHAGUZI MKUU 2025

Walimu ni nguzo ya maendeleo ya taifa, kwani wao ndio wanaoandaa kizazi chenye maarifa na maadili. Kadri tunavyokaribia uchaguzi mkuu wa 2025, ushiriki wao katika mchakato wa kidemokrasia ni muhimu ili kuhakikisha taifa linapata viongozi wanaotanguliza elimu kama msingi wa maendeleo.


Viongozi bora watasaidia kuendeleleza sekta hii ambayo kwa kiasi kikubwa imepiga hatua kimaendeleo. Pamoja na mafanikio yaliyopo bado tunahitaji kuendelea kuboresha mazingira mbalimbali kama miundombinu ya shule, kukuza matumizi ya teknolojia, na kusimamia haki za walimu. Ili haya yawezekane, wanahitaji viongozi

wanaoona elimu kama injini ya maendeleo ya taifa. Hivyo basi, kura za walimu ni nyenzo ya kuhakikisha mwelekeo huo unaendelea kuwepo kwenye ajenda kuu ya kitaifa.

Hivyo basi, tunatoa wito kwa walimu wote kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu wa 2025, si kwa kupiga kura pekee bali pia kwa kuelimisha wanafunzi na jamii kuhusu umuhimu wa amani, mshikamano na uwajibikaji wa kiraia. Kwa kufanya hivyo, walimu watakuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa utulivu na taifa linaendelea kusonga mbele.

Mungu ibariki Tanzania

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz

Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

NAIBU KATIBU WAKUU OR-TAMISEMI WATEMBELEA BANDA LA TSC SIKU YA KILELE CHA NANENANE

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Naibu Katibu Wakuu wa Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Sospeter Mtwale anayeshughulikia Serikali za Mitaa, Mhandisi Rogatus Mativika anayeshughulikia miundombinu, na Prof. Tumaini Nagu anayeshughulikia afya, wamembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 8 Agosti 2025, ikiwa ni siku ya kilele cha Maonesho ya Wakulima ya Nanenane Kitaifa yanayofanyika katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Katika ziara hiyo, viongozi hao walipata maelezo kuhusu huduma zinazotolewa na TSC, ikiwemo ajira, upandishwaji vyeo, na masuala ya nidhamu kwa walimu, sambamba na juhudi za Tume katika kusogeza huduma karibu na walimu na wadau wa elimu nchini.

Viongozi hao wameipongeza Tume kwa kazi nzuri wanayoifanya, ikiwemo kushughulikia changamoto mbalimbali za walimu. Wameeleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa



Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI anayeshughulikia miundombinu, Mhandisi Rogatus Mativika (wa tatu kutoka kushoto) akizungumza na mmoja wa maafisa wa TSC wakati wa ziara yao kwenye maonesho ya Nanenane Kitaifa.

Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya jitihada kubwa katika kushughulikia maslahi ya walimu, hatua inayoongeza morali na kuimarisha ubora wa elimu nchini. Maonesho ya mwaka huu

yamebeba kaulimbiu isemayo "Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi" na yamehudhuriwa na washiriki kutoka mikoa mbalimbali.



Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI anayeshughulikia afya, Prof. Tumaini Nagu (kushoto) akimsikiliza mtoa huduma (hayupo pichani) kwenye banda la TSC wakati wa Maonesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa jijini Dodoma.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini TSC, Bw. Artemony Vincent akitoa maelezo kwa Viongozi wa OR-TAMISEMI kuhusu huduma zinazotolewa na Tume katika maonesho ya Nanenane jijini Dodoma.

TSC YAKUTANA NA UONGOZI WA CWT NGAZI YA TAIFA KUIMARISHA HUDUMA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 22 Agosti, 2025 imefanya kikao na Uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ngazi ya Taifa jijini Dodoma, kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika utoaji wa huduma bora kwa walimu.

Kikao hicho kiliongozwa na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, ambaye alisisitiza kuwa CWT, kama chombo cha walimu nchini, ni mda muhimu katika kuhakikisha walimu wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia miiko na maadili ya kazi hiyo.

"CWT ni mshirika mkubwa wa TSC. Lengo letu ni kuhakikisha walimu wanahudumiwa kwa ubora zaidi, wakiwa na uelewa wa kutosha juu ya wajibu wao kazini ili kuepusha ukiukaji wa taratibu za utumishi," alisema Mwl. Nkwama.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Elimu na Mafunzo Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Bi



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (Katikati) akiongoza kikao cha Menejimenti ya TSC na ujumbe kutoka Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ngazi ya Taifa kilichofanyika tarehe 22 Agosti, 2025 jijini Dodoma.

Stella Kiabo aliipongeza Tume kwa kushirikisha chama hicho katika masuala yanayohusu maendeleo ya walimu, akisisitiza kuwa mshikamano

huo utaboresha maslahi na ari ya walimu nchini.

"TSC na CWT tukishirikiana kwa karibu, walimu watanufaika zaidi kwa kupata huduma stahiki na haki zao za msingi. Ushirikiano huu pia utasaidia kutatua changamoto zinazowakabili walimu kwa haraka zaidi," alisema Bi Kiabo.

Aidha, viongozi wa pande zote mbili walisema kuwa, ili kufanikisha malengo ya elimu nchini, ni muhimu kushirikiana kwa nguvu zote:

"Wote tunamlenga mwalimu, hivyo tunahitaji nguvu ya pamoja kuhakikisha mwalimu anatimiza wajibu wake na kupata haki zake," walieleza.

CWT pia wamepongeza Tume kwa kuwa na sala ambayo hufanyika kabla ya kuanza kwa shughuli rasmi siku husika, ikichangia kuimarisha maadili, haki na uwajibikaji wa watumishi wa Tume katika kutekeleza majukumu yao.

Kupitia kikao hiki, pande zote mbili zimeahidi kuendeleza mashauriano ya mara kwa mara ili kujenga mazingira rafiki ya utumishi, kuongeza ufanisi wa walimu kazini, na hatimaye kuinua ubora wa elimu nchini.



Mkuu wa Idara ya Elimu na Mafunzo Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Bi Stella Kiabo akizungumza katika kikao na Menejimenti ya TSC, jijini Dodoma, tarehe 22 Agosti, 2025.

TSC YAKUTANA NA UONGOZI WA CWT NGAZI YA TAIFA KUIMARISHA HUDUMA KWA WALIMU



Wajumbe Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa kwenye kikao na Ujumbe wa CWT (hawapo pichani), tarehe 22 Agosti, 2025.



Washiriki kutoka Chama cha Walimu Tanzania wakiwa kwenye kikao na Wajumbe wa Menejimenti ya TSC (hawapo pichani), jijini Dodoma, tarehe 22 Agosti, 2025.



Kikao kati ya Menejimenti ya TSC na CWT kikiwa kinaendelea jijini Dodoma tarehe 22 Agosti, 2025.

MAFUNZO YAWAPA NGUVU WAJUMBE WA TSC LUSHOTO KUSIMAMIA NIDHAMU YA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Lushoto

Mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) yamewajengea uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Walimu, na yamepunguza mvutano wakati wa kushughulikia mashauri ya kinidhamu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Lushoto, Bw. Abihudi Simon Hemba, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini alipokuwa akieleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kutatua changamoto za walimu.

Bw. Hemba alisema kuwa mafunzo kwa Wakuu wa Shule yamechangia kupunguza idadi ya mashauri ya kinidhamu kwa kuwa makosa madogo yanashughulikiwa ngazi ya shule, jambo linalosaidia walimu kurekebisha mapema bila kufikishwa kwenye vikao vya Tume.

Aidha, alieleza kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewapandisha vyeo jumla ya walimu 1,705, wakiwemo 1,123 wa shule za msingi na 682 wa shule za sekondari. Vilevile, Serikali imejitahidi kupunguza tatizo la upungufu wa walimu kwa kutoa ajira mpya 241, kati yao 135 ni wa shule za msingi na 106 ni wa shule za sekondari.

Kuhusu masuala ya maslahi ya walimu, Bw. Hemba alisema Serikali imeendelea kulipa madeni ya likizo na matibabu kwa wakati, huku madai ya malimbikizo ya mishahara yakishughulikiwa na taarifa zake kutumwa Makao Makuu ya Utumishi kupitia mfumo rasmi.

Alibainisha kuwa mafanikio mengine ni pamoja na kuiwezesha Ofisi ya TSC Wilaya ya Lushoto kupata vitendea kazi ikiwemo pikipiki na kuendelea kuendesha mafunzo kwa watumishi.

Bw. Hemba alisisitiza kuwa TSC

inatambua nafasi ya mwalimu kama kioo cha jamii na muongoza njia, hivyo aliwataka walimu kuwa mfano wa kuigwa kwa kuzingatia sheria, hususan katika kipindi cha uchaguzi, na kuwaelimisha wananchi kushiriki uchaguzi ujao kwa amani na utulivu.

Katika hatua nyingine, alisema TSC Lushoto imekuwa ikitoa elimu mashuleni kwa kuwatembelea walimu, kuwapa ushauri nasaha na kushauriana na waajiri kuhusu kuwabadilishia vituo vya kazi inapohitajika.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lushoto, Bw. Abihudi Simon Hemba.

TSC YATEMBELEA UJENZI WA MAKAO MAKUU MAPYA NJEDENGWA

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanya ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu ya Tume katika eneo la Njedengwa, jijini Dodoma, Agosti 14, 2025.

Ziara hiyo ni utekelezaji wa maelekezo ya Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma yaliyotolewa katika kikao chake kilichofanyika Agosti 13, 2025 jijini Dodoma.

Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, aliongoza timu ya menejimenti katika ukaguzi huo, akieleza kuwa lengo ni kujionea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo muhimu kwa Tume.

Katika ziara hiyo, menejimenti ilikutana na mkandarasi wa mradi huo, SUMA JKT, ambapo ilielezwa kuwa ujenzi unaendelea vizuri na shughuli mbalimbali za ujenzi zinafanyika kwa kasi.

Hata hivyo, menejimenti ilisisitiza umuhimu wa kuongeza spidi ya utekelezaji ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kufikia Desemba 2025 kama ilivyopangwa.

Ujenzi wa Makao Makuu mapya ya TSC unatarajiwa kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Tume.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiongoza kikao kati ya Menejimenti ya Tume na Mkandarasi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Tume, SUMA JKT, wakati wa ukaguzi wa ujenzi huo uliofanywa na Menejimenti ya TSC tarehe 14 Agosti, 2025.



Washiriki wa kikao kati ya Menejimenti ya Tume na Mkandarasi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Tume, SUMA JKT, wakati wa ukaguzi wa ujenzi huo uliofanywa na Menejimenti ya TSC tarehe 14 Agosti, 2025 wakiwa kwenye kikao hicho.

TSC YATEMBELEA UJENZI WA MAKAO MAKUU MAPYA NJEDENGWA



Sehemu ya jengo jipya la Makao Makuu ya Tume linaloendelea kujengwa na Mkandarasi SUMA JKT katika eneo la Njedengwa, Dodoma.



Menejimenti ya TSC ikikagua hatua za ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Tume, Agosti 14, 2025.

PROF. MURUKE AKABIDHI MWONGOZO KWA MAKAMISHNA WA TUME

Mwongozo huo unalenga kuwajengea uelewa walimu wapya kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo utumishi wao.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaoajiriwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama tarehe 19 Agosti, 2025 jijini Dodoma.

Na Mwandishi Wetu, Dodoma.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke, tarehe 19 Agosti 2025 amekabidhi Kitabu cha Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaoajiriwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa Katibu na Makamishna wa Tume jijini Dodoma.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Muruke alisema Mwongozo huo ni nyenzo muhimu ya kitaaluma na kiutumishi kwa walimu wapya, ili kuhakikisha wanazingatia miiko, maadili na taratibu za kazi yao mara baada ya kuajiriwa.

"Mwongozo huu umeandaliwa mahsusi na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa lengo la kuwajengea uelewa walimu wapya kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma. Tunataka mwalimu mpya aingie kazini akiwa na mwongozo sahihi wa namna ya kutekeleza wajibu wake kwa nidhamu na uadilifu," alisisitiza Prof. Muruke.

Mwongozo huo unafafanua kwa kina masuala ya haki na wajibu wa watumishi wa umma, mbinu bora za utendaji kazi, utunzaji wa kumbukumbu, na misingi ya utoaji wa huduma bora kwa wanafunzi na jamii. Pia unaeleza hatua za kinidhamu, taratibu za kupanda vyeo, pamoja na wajibu wa walimu katika kudumisha maadili

na heshima ya taaluma ya ualimu.

Kwa mujibu wa Tume, lengo kuu la mwongozo huu ni kuhakikisha walimu wapya wanaingia kazini wakiwa na maarifa sahihi yanayowawezesha kutoa mchango bora katika kuimarisha sekta ya elimu na kufanikisha malengo ya kitaifa na kimataifa ya maendeleo ya elimu.

Taratibu za kusambaza Mwongozo huo shuleni zinaendelea, na tayari unapatikana kupitia tovuti ya Tume: www.tsc.go.tz. Ni matarajio ya Tume kuwa mwongozo huu utakuwa dira ya walimu wapya katika kujenga nidhamu, uadilifu na ari ya kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaoajiriwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa mmoja wa Makamishna wa Tume, Mwl. Jane Mtindya tarehe 19 Agosti, 2025 jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaoajiriwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa mmoja wa Makamishna wa Tume, Bi. Mariam Mwanikwa tarehe 19 Agosti, 2025 jijini Dodoma.

PROF. MURUKE AKABIDHI MWONGOZO KWA MAKAMISHNA WA TUME



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaojirwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa mmoja wa Makamishna wa Tume, Bi. Mariam Haji tarehe 19 Agosti, 2025 jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaojirwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa mmoja wa Makamishna wa Tume, Mwl. Lameck Mahewa tarehe 19 Agosti, 2025 jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaojirwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa mmoja wa Makamishna wa Tume, Bw. Agrey Mleli tarehe 19 Agosti, 2025 jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) akipokea Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaojirwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kutoka kwa mmoja wa Makamishna wa Tume, Bi. Mariam Mwanikwa tarehe 19 Agosti, 2025 jijini Dodoma.

PROF. MURUKE AKABIDHI MWONGOZO KWA MAKAMISHNA WA TUME



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaoajiriwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa Katibu wa Chama cha Walimu (CWT) Mkoa wa Kagera, Bw. Njile Anthony Lufasinza tarehe 20 Agosti, 2025 jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaoajiriwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa Katibu wa Chama cha Walimu (CWT) Wilaya ya Ngara, Bw. Amani Zephania Msanga tarehe 20 Agosti, 2025 jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaoajiriwa Katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara Makamu Mwenyekiti wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa tarehe 20 Agosti, 2025 jijini Dodoma.

WALIMU WILAYANI MAFIA WATAKIWA KUJITOKEZA KWA WINGI KUSHIRIKI UCHAGUZI MKUU UJAO



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mafia, Mwl. Zaituni J. Sing'ombe.

Mafanikio ya Serikali

Akizungumzia mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, Mwl. Zaituni alisema TSC Wilaya ya Mafia inajivunia hatua zilizochukuliwa katika kushughulikia kero za walimu, ikiwemo ulipaji wa madeni ya mishahara, likizo, fedha za uhamisho na kupandishwa madaraja.

Alisema pia Serikali imeendelea kutoa ajira mpya kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kupitia ujenzi na ukarabati wa nyumba za walimu na vyumba vya madarasa.

Kwa mujibu wa Mwl. Zaituni, walimu 37 kati ya 61 waliostahili kupandishwa madaraja hadi kufikia tarehe 30 Julai tayari wamepandishwa vyeo, hatua iliyoongeza hamasa ya kufanya kazi kwa bidii.

Mafunzo ya TSC

Kwa upande wake, Afisa Ajira wa TSC Wilaya ya Mafia, Bw. Hamad F. Hamad, aliipongeza Serikali kwa kuwawezesha kutoa mafunzo ya usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa Maafisa wa Tume.

Alisema mafunzo hayo yameleta matokeo chanya kwa kuwa yameimarisha uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi, yameongeza uwezo wa kuchambua mashauri kwa kina, kuzuia makosa ya kinidhamu na kuboresha uandishi wa taarifa za mashauri.

Aidha, alisema mafunzo kwa Wakuu wa Shule yamewakumbusha kuwa nao ni sehemu ya mfumo wa uwajibikaji, na hivyo wanapaswa kuwa mfano wa kuigwa katika maadili ya kazi, jambo linalowasaidia kuwa makini zaidi katika usimamizi wao.

Na Mwandishi Wetu – Mafia.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mafia imetoa wito kwa walimu wa shule za msingi na sekondari kujitokeza kwa wingi kushiriki katika upigaji kura kwenye Uchaguzi Mkuu ujao.

Wito huo umetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mafia, Mwl. Zaituni J. Sing'ombe, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini alipokuwa akieleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kushughulikia changamoto za walimu.

Mwl. Zaituni alisema kuwa mwaka huu kutakuwa na uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, hivyo ni muhimu walimu wakatumia haki yao ya kupiga kura. Alisisitiza kuwa walimu hawapaswi kuonyesha ushabiki wa kisiasa wakiwa katika maeneo ya kazi.

"Siku ya uchaguzi walimu wanapaswa kwenda kupiga kura kwa amani na baadaye kurejea nyumbani kusubiri matokeo yatakayotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi," alisema.

Aliongeza kuwa walimu, kama sehemu ya jamii, wanapaswa kutumia nafasi zao kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa amani na mshikamano kabla, wakati na baada ya uchaguzi.



Afisa Ajira wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mafia, Bw. Hamad F. Hamad.

KIKAO CHA KAMATI YA AJIRA NA MAENDELEO YA WALIMU CHAFANYIKA DODOMA

Na Mwandishi Wetu – Kibondo

Kikao cha Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu cha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kimefanyika tarehe 12 Agosti, 2025, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Mkutano wa Tume.

Kikao hicho, kilichofanyika katika Ofisi za Tume jijini Dodoma, kiliongozwa na mmoja wa Makamishna wa TSC, Bw. Aggrey Mleli, ambapo wajumbe walijadili masuala mbalimbali yanayohusu ajira na maendeleo ya walimu nchini.

Akizungumza katika kikao hicho, Mwenyekiti wa kikao Bw. Aggrey Mleli alipongeza juhudi na kazi nzuri inayotekelezwa na Tume katika kusimamia ajira na maendeleo ya walimu kote nchini.

Kwa upande wake, Katibu wa Tume, Mwalimu Paulina Nkwama, alitoa ufafanuzi wa kina juu ya masuala mbalimbali yanayohusu ajira na maendeleo ya walimu, akibainisha hatua zinazochukuliwa na Tume katika kuboresha huduma kwa walimu.

Kikao hiki kinatarajiwa kuchangia katika maandalizi bora ya Mkutano wa Tume, kwa kuhakikisha kuwa masuala ya ajira na maendeleo ya walimu yanapewa kipaumbele ili kuimarisha elimu nchini.



Kikao cha Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya Tume ya Utumishi wa Walimu kikiongozwa na Kamishna wa Tume, Bw. Aggrey Mleli tarehe 12 Agosti, 2025 kikiwa kinaendelea katika ofisi za TSC Makao Makuu jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (kulia) na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya wakiwa katika kikao cha Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu tarehe 12 Agosti, 2025 katika ofisi za Tume jijini Dodoma.



Kikao cha Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya Tume ya Utumishi wa Walimu kikiongozwa na Kamishna wa Tume, Bw. Aggrey Mleli tarehe 12 Agosti, 2025 kikiwa kinaendelea katika ofisi za TSC Makao Makuu jijini Dodoma.

KIKAO CHA KAMATI YA AJIRA NA MAENDELEO YA WALIMU CHAFANYIKA DODOMA



Washiriki wa kiko cha Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu wakiwa kwenye kikao hicho tarehe 12 Agosti, 2025 katika ofisi za Tume jijini Dodoma.

MAFUNZO ELEKEZI KWA WAJUMBE WA TSC KIGAMBONI YAWAJENGEA UWEZO KUTOA MAAMUZI YA KINIDHAMU

Na Mwandishi Wetu – Kigamboni

Mafunzo elekezi kwa Wakuu wa Shule na Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigamboni yamewajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura ya 448, hususan katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu ya walimu.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kigamboni, Bi. Arodia Rweshabura, alisema hayo hivi karibuni wakati akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika utatuzi wa changamoto zinazowakabili walimu.

Bi. Rweshabura alisema kuwa mafunzo hayo yameleta matokeo chanya kwa wajumbe, kwani yamewawezesha kuwa makini zaidi katika mijadala na kufanya maamuzi yenye kuzingatia misingi ya sheria na taratibu.

“Kwa kutumia uelewa waliouputa kupitia mafunzo haya, wajumbe wamekuwa wakijadili kwa kina na kwa uangalifu mkubwa kabla ya kuamua mashauri ya kinidhamu ya walimu,” alisisitiza.

Aidha, alisema Wakuu wa Shule waliopatiwa mafunzo wamekuwa mabalozi wa Tume kwa kuwaelimisha walimu wenzao juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma ili kuepuka kuingia kwenye mashauri ya kinidhamu.

Kwa mujibu wake, mafunzo hayo yamewawezesha Wakuu wa Shule kutambua nafasi yao kama mamlaka ya nidhamu katika ngazi ya shule, kuwashauri na kuwaelekeza walimu kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

“Utoaji wa ushauri ni hatua ya kwanza muhimu katika kumsaidia mwalimu kuboresha mwenendo



Kaimu Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigamboni, Bi. Arodia Rweshabura.

wake wa kazi, na hatua hii imesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa mashauri ya kinidhamu,” aliongeza Bi. Rweshabura.

Mafanikio ya Kigamboni

Katika hatua nyingine, Bi. Rweshabura aliishukuru Serikali kwa kuendelea kutatua changamoto zinazowakabili walimu wa Kigamboni, ambapo walimu 88 wa shule za sekondari na 73 wa shule za msingi walipandishwa vyeo, huku wilaya hiyo ikipokea walimu wapya 73 na wataalamu wa maabara 2, na hivyo kufanya jumla ya walimu

wapya waliopokelewa kufikia 75.

Aliongeza kuwa, kwa lengo la kuzuia walimu wengi kuingia kwenye mashauri ya kinidhamu, Tume imekuwa ikifanya ziara za mafunzo mashuleni ili kutoa elimu ya haki, wajibu na maadili ya kazi.

“Tunatumia mbinu ya mazungumzo ya ana kwa ana ambapo tunawapa walimu elimu ya kisheria na kimaadili. Pia tunawashauri namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha zinazoweza kuathiri utendaji wao wa kazi,” alisema.

MAFUNZO ELEKEZI KWA WAJUMBE WA TSC KIGAMBONI YAWAJENGEA UWEZO KUTOA MAAMUZI YA KINIDHAMU



Picha ya pamoja ya washiriki wa mafunzo.



Kaimu Katibu Msaidizi TSC Kigamboni, Bi. Arodia Rweshabura (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa anayeshughulikia Ajira na Maendeleo ya Walimu, Bi. Jesca D. Kwalevele (kushoto) na Afisa anayeshughulikia Nidhamu na Maadili, Bw. Melkizedeck D. Ruambo (kulia). walimu wa Shule ya Msingi Idumulavani baada ya kutoa elimu.

Kaimu Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigamboni Bi. Arodia Rweshabura (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Anayeshughulikia Ajira na Maendeleo ya Walimu, Bi. Jesca D. Kwalevele (katikati) na Afisa anayeshughulikia Nidhamu na Maadili, Bw. Melkizedeck D. Ruambo (kulia).

TSC KUENDELEA KUIMARISHA NIDHAMU NA MAADILI YA WALIMU

Na Mwandishi wetu.

DODOMA, Agosti 12, 2025 – Tume ya Utumishi wa Walimu inaendelea kuimarisha nidhamu na maadili kwa walimu nchini, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuinua ubora wa elimu.

Hayo yamebainika katika kikao cha Kamati ya Tume ya Maadili na Nidhamu kilichofanyika katika Ofisi za Tume Makao Makuu jijini Dodoma, kikiongozwa na mmoja wa Makamishna wa Tume, Mwl. Lameck Mahewa.

Kikao hicho kilikuwa ni sehemu ya maandalizi ya Mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni.

Katika kikao hicho, wajumbe walijadili kwa kina mikakati ya kuhakikisha walimu wanazingatia maadili ya kazi, kufuata kanuni na taratibu za utumishi wa umma, na kuepuka vitendo vinavyoweza kudhoofisha taaluma ya ualimu.

Mwl. Mahewa aliipongeza Ofisi ya Katibu wa Tume kwa ushughulikiaji wa haraka wa rufaa za walimu, akisema hatua hiyo “ni msingi wa utoaji wa haki na nguzo ya kuimarisha imani ya walimu kwa Tume yao.”

Aidha, alisisitiza kuwa maadili na nidhamu ya walimu ni jambo lisilopaswa kupuuzwa kwani linaathiri moja kwa moja ubora wa elimu nchini.

Tume ya Utumishi wa Walimu imejipanga kuendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma, ili kuongeza uwajibikaji na kuboresha huduma kwa wanafunzi.



Kikao cha Kamati ya Maadili na Nidhamu kikiendelea chini ya uenyekiti wa Mwl. Lameck Mahewa, tarehe 12 Agosti, 2025, katika Ofisi za Tume Makao Makuu, Dodoma.



Washiriki wa Kikao cha Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakiendelea na majadiliano, tarehe 12 Agosti, 2025, katika Ofisi za Tume Makao Makuu, Dodoma.

TSC KUENDELEA KUIMARISHA NIDHAMU NA MAADILI YA WALIMU



Sehemu ya washiriki wa kikao cha Kamati ya Tume ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakiendelea na majadiliano, tarehe 12 Agosti, 2025, katika Ofisi za Tume Makao Makuu, Dodoma.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Mectildis Kapinga (kushoto), akijadili jambo na Afisa Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Selina Magoiga, wakati wa kikao cha Kamati ya Maadili na Nidhamu kilichofanyika tarehe 12 Agosti, 2025, katika Ofisi za Tume Makao Makuu, Dodoma.



Mwenyekiti wa kikao cha Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Lameck Mahewa, akihitimisha kikao kilichofanyika tarehe 12 Agosti, 2025, katika Ofisi za Tume Makao Makuu, Dodoma.

SERIKALI YA AWAMU YA SITA YAIMARISHA MAZINGIRA YA KAZI KWA WALIMU KINONDONI



Na Mwandishi wetu, Kinondoni.

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kinondoni imepongeza jitihada za Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuimarisha mazingira ya utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kinondoni, Bw. Theobard Kilindo, ameeleza kuwa Serikali imewezesha ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kutoa vitendea kazi muhimu pamoja na kuwezesha kufanyika kwa vikao vinne vya kisheria katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Aidha, Serikali imewezesha ofisi hiyo kupata huduma za mtandao kutoka Kampuni ya Mawasiliano ya Serikali (TTCL), jambo lililorahisisha upatikanaji wa intaneti na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Pia, imewezesha upatikanaji wa usafiri wa pikipiki na kutoa mafunzo kwa walimu wapya 152.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, walimu 333 wa Manispaa ya Kinondoni wamepandishwa vyeo, wakiwemo walimu 209 wa shule za msingi na walimu 124 wa shule za sekondari. Vilevile, walimu 1,720 wamepatiwa malipo ya fedha za likizo yenye jumla ya shilingi milioni 532, ambapo milioni 200 ni fedha za ruzuku na milioni 332 zimetokana na mapato ya ndani.

Bw. Kilindo alisisitiza pia umuhimu wa walimu kushiriki katika uchaguzi ujao wa Oktoba, akibainisha kuwa ni haki ya kikatiba. "Tulifanya kikao mapema mwaka huu na



walimu 1,436 ambapo tuliwahimiza kushiriki kikamilifu katika zoezi la kupiga kura," alisema.

Aidha, zaidi ya walimu 1,675 wamejengewa uwezo katika uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma kupitia semina na mikutano ya kikazi kwa kushirikiana na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na waajiri.

Kwa sasa Wilaya ya Kinondoni ina shule za msingi 84 na sekondari 36 zenye jumla ya walimu 2,982, kati yao walimu 2,021 ni wa shule za msingi na 961 wa shule za sekondari.

KAMATI YA UTAWALA, FEDHA, UTAFITI NA ELIMU KWA UMMA YAWEKA MIKAKATI KABLA YA MKUTANO WA TUME

Na Mwandishi wetu.

DODOMA, Agosti 13, 2025 – Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu imekutana kujadili masuala muhimu ya utendaji wa Tume, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Mkutano wa Tume unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Kikao hicho, kilichoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Bi. Mariam Mnilwa, kiliwaleta pamoja wajumbe na watendaji wa Tume kujadili utekelezaji wa shughuli za idara na vitengo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti, majadiliano hayo yamelenga kuhakikisha mipango na mikakati ya Tume inatekelezwa kwa ufanisi, hususan katika maeneo ya utawala, usimamizi wa fedha, utafiti na elimu kwa umma.

Kamati hii ina jukumu la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa masuala ya kiutawala ya Tume, kuhakikisha rasilimali zinatumiwa ipasavyo na kwamba wananchi, hususan walimu, wanapewa taarifa sahihi kuhusu huduma zinazotolewa na Tume.



Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Mariam Mnilwa (kushoto) akiongoza kikao cha Kamati hiyo kilichofanyika tarehe 13 Agosti, 2025 jijini Dodoma. Pichani, upande wa kulia ni Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama.



Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimalivatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Zachary Dida akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume wakati wa kikao cha Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu iliyofanyika tarehe 13 Agosti, 2025 jijini Dodoma.



Baadhi ya washiriki wa kikao cha Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakiendelea na kikao.

KAMATI YA UTAWALA, FEDHA, UTAFITI NA ELIMU KWA UMMA YAWEKA MIKAKATI KABLA YA MKUTANO WA TUME



SIKU YA KILELE CHA MAONESHU YA NANENANE: KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU ATEMBELEA BANDA LA TSC

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, tarehe 8 Agosti 2025 ametembelea maonesho ya Wakulima ya Nanenane Kitaifa yanayofanyika katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma, ikiwa ni siku ya kilele cha maadhimisho hayo.

Mgeni rasmi katika kilele cha maonesho hayo alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye aliongoza hafla hiyo iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, sekta binafsi na wananchi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Akiwa katika banda la Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Nkwama alitoa huduma mbalimbali kwa wananchi na wadau wa elimu waliotembelea banda hilo, zikiwemo ushauri wa masuala ya ajira, upandishwaji vyeo na taratibu za nidhamu kwa walimu.

Maonesho ya mwaka huu yamebeba kaulimbiu isemayo "Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi" ikilenga kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi ili kuchagua viongozi wenye maono ya kuendeleza sekta hizo muhimu kwa ustawi wa Taifa.

Kwa siku nane mfululizo, TSC iliweka kambi katika viwanja hivyo, ikitoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupokea na kushughulikia malalamiko kutoka kwa walimu na wananchi, sambamba na kutoa elimu kuhusu majukumu na huduma zinazotolewa na Tume hiyo.

Mwl. Nkwama alieleza kuwa ushiriki wa TSC katika maonesho hayo ni fursa muhimu ya kukutana na walimu na wadau ana kwa ana, jambo linalosaidia kuongeza uelewa wa jamii kuhusu haki, wajibu na taratibu za utumishi wa walimu nchini.



Huduma kwa vitendo: Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akihudumia wateja katika banda la TSC, siku ya kilele cha maadhimisho ya Nanenane.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAPONGEZWA KWA MAFUNZO YA WAJUMBE WA KAMATI ZA AJIRA, UPANDISHAJI VYEO NA NIDHAMU

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imepongezwa kwa hatua yake ya kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu kwa ngazi ya wilaya, hatua inayochukuliwa kuwa kichocheo cha haki na uwazi katika kusimamia utumishi wa walimu nchini.

Pongezi hizo zilitolewa tarehe 6 Agosti, 2025 na Katibu Tawala wa Wilaya ya Chemba, Bi. Sarah John, pamoja na Katibu Tawala wa Wilaya ya Kongwa, Bi. Sozi Ngate, walipotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Wakulima ya Nanenane yanayofanyika Kitaifa katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Viongozi hao walieleza kuwa Tume imeendelea kufanya kazi nzuri ya kutoa huduma kwa walimu, na kuongeza kuwa mafunzo yanayotolewa kwa wajumbe wa kamati hizo ni msingi muhimu wa kuhakikisha maamuzi yanayotolewa yanazingatia sheria, kanuni na misingi ya haki.

“Tunapongeza jitihada za Tume kwa kuona umuhimu wa kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati hizi nyeti.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Chemba, Bi. Sarah John (wa pili kutoka kushoto mwenye kofia) akizungumza katika banda la TSC kwenye maonesho ya Nanenane jijini Dodoma.

Mafunzo haya ni ya msingi kwa kuwa yanawawezesha kufanya maamuzi kwa weledi na haki,” alisema Bi. Sarah John.

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura ya 448 na Kanuni zake za mwaka 2016, Katibu Tawala wa Wilaya ni mjumbe wa Kamati ya Ajira, Upandishwaji Vyeo

na Nidhamu katika Wilaya husika, hivyo ni muhimu kwa viongozi hao kuwa na uelewa mpana wa majukumu yao.

Bi. Sozi Ngate alisisitiza kuwa dhamira ya Tume katika kutoa hudumabora kwa walimu na viongozi wa elimu imeonekana wazi kupitia mafunzo haya, huku akihimiza kuwa jitihada zaidi zifanyike kuhakikisha kuwa makatibu tawala wote nchini wanapatiwa mafunzo hayo.

“Kwa kuwa baadhi yetu hatujapata mafunzo haya, tunaomba Tume iendelee na juhudi zake ili kuhakikisha wajumbe wote wa Kamati hizi wanapitia mafunzo haya muhimu. Hii itasaidia kuongeza ufanisi na uadilifu katika kusimamia masuala ya ajira, upandishwaji vyeo na nidhamu kwa walimu,” alisema Bi. Ngate.

Tume ya Utumishi wa Walimu imekuwa ikishiriki kikamilifu katika maonesho ya Nanenane kwa lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya majukumu yake, huduma zinazotolewa kwa walimu pamoja na kueleza nafasi ya kamati za ajira na nidhamu katika uendeshaji wa masuala ya kiutumishi kwa walimu wa shule za msingi na sekondari za serikali.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Kongwa, Bi. Sozi Ngate (mwenye koti la kijani) akisikiliza maelezo kutoka kwa watoa huduma alipotembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu kwenye maonesho ya Nanenane jijini Dodoma.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YAPONGEZWA KWA MAFUNZO YA WAJUMBE WA KAMATI ZA AJIRA, UPANDISHAJI VYEO NA NIDHAMU



Wateja mbalimbali wakihudumiwa kwenye banda la TSC kwenye maonesho ya Nanenane jijini Dodoma.

TSC YAWAAGA WACHEZAJI WANAOKWENDA SHIMIWI MWANZA



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama, akizungumza na wachezaji pamoja na watumishi wa Tume wakati wa hafla ya kuwaga wachezaji wanaoshiriki mashindano ya Shimiwi Mwanza.

Na Mwandishi wetu, Dodoma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, tarehe 29 Agosti 2025, amewaaga rasmi wachezaji wa Tume watakaoshiriki mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yanayotarajiwa kufanyika jijini Mwanza.

Akizungumza katika hafla fupi iliyofanyika katika ukumbi wa

Tume, Makao Makuu, Mwl. Nkwama aliwataka washiriki hao kuzingatia miiko na maadili ya Utumishi wa Umma katika kipindi chote cha michezo hiyo.

"Haijawahi kutokea na wala sitarajii kusikia kwa upande wetu kuwa mtumishi wa Tume anajihusisha na vitendo vinavyokiuka maadili ya utumishi wa umma. Hakikisheni mnazingatia malengo yaliyowapeleka huko," alisema Katibu huyo.

Timu ya TSC yenye zaidi ya

wachezaji 14 itashiriki michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa pete, kurusha tufe, mbio za baiskeli, riadha, bao na draft.

Katika hatua nyingine, Katibu wa Tume alipokea kikombe na medali kutoka kwa washindi wa mashindano ya Mei Mosi mwaka huu. Miongoni mwa washindi hao ni Pulkeria Mwaimu, aliyenyakua kombe katika mchezo wa draft kwa upande wa wanawake, na Enid Geoffrey, aliyeshika nafasi ya pili katika mchezo wa kurusha tufe.

Mwl. Nkwama aliwapongeza washindi hao akikabidha kuwa wameitangaza vyema Tume kupitia michezo, huku akihimiza watumishi wote wa Tume kupenda michezo na kufanya mazoezi mara kwa mara kwa ajili ya kujenga afya bora.

Awali, Mwenyekiti wa Michezo wa TSC, Mwl. Mectildis Kapinga, alieleza kuwa wanamichezo wengine wa Tume walioshiriki katika michezo ya Mei Mosi licha ya kutopata vikombe na medali walifanya vizuri kwa kuingia katika kumi bora kwenye michezo waliyoshiriki.

Aidha, mchezaji Debora Chambo akitoa neno la shukrani alisema, "Tunaishukuru Menejimenti ya Tume kwa kuipa michezo kipaumbele. Wachezaji wote tuna ari kubwa ya mashindano haya, na matarajio yetu ni kufanya vizuri na kuiletea Tume ushindi."

Mashindano ya SHIMIWI yanatarajiwa kutoa fursa ya kuonyesha vipaji vya michezo pamoja na kukuza afya na mshikamano miongoni mwa watumishi wa umma.



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akipokea kikombe cha ushindi kutoka kwa mshindi wa mchezo wa draft katika mashindano ya Mei Mosi ya mwaka 2025, Bi. Pulkeria Mwaimu (katikati) katika hafla iliyofanyika TSC Makao Makuu Dodoma tarehe 29 Agosti, 2025. Pichani upande wa kulia ni Mwenyekiti wa Michezo wa Tume, Mwl. Mectildis Kapinga.

TSC YAWAAGA WACHEZAJI WANAOKWENDA SHIMIWI MWANZA



Katibu TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akipokea medali kutoka kwa mshindi wa pili kwenye mchezo wa kurusha tufe wanawake katika mashindano ya Meimosi ya mwaka 2025, Enid Geofrey katika hafla iliyofanyika TSC Makao Makuu Dodoma tarehe 29 Agosti, 2025.



Washiriki wa hafla ya kuwaga wachezaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa ajili ya kusafiri mkoani Mwanza kushiriki mashindano ya Shimizvi liyofanyika tarehe 29 Agosti, 2025 TSC Makao makuu wakiwa katika hali ya utulivu.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wachezaji wa Tume wakati wa hafla ya kuwaga kwa ajili ya kusafiri mkoani Mwanza kushiriki mashindano ya Shimizvi.



Mwenyekiti wa Michezo wa Tume Mwl. Mecktildis Kapinga, Mwenyekiti akitoa neno la utangulizi wakati wa hafla ya kuwaga wanamichezo wa tume wanaokwenda kushiriki mashindano ya Shimizvi mkoani Mwanza.

TSC YAWAAGA WACHEZAJI WANAOKWENDA SHIMIWI MWANZA



Wachezaji na baadhi ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi wa TSC.



Wachezaji wa TSC wakiwa katika hali ya furaha, wakionyesha mshikamano na ari kubwa kabla ya kuelekea mkoani Mwanza kushiriki mashindano ya Shimiwi.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu